

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Simu: +255-26- 2323189  
Nukushi:  
Barua pepe: [ps@moha.go.tz](mailto:ps@moha.go.tz)  
Tovuti: [www.moha.go.tz](http://www.moha.go.tz)



Taasisi ya Asha Rose Migiro  
Chuo Kikuu cha Dodoma  
S.L. P. 2916  
40483 Dodoma

13 /07/2018

**TAARIFA KWA UMMA**

**WAKIMBIZI WOTE WALIO NJE YA KAMBI ZA  
WAKIMBIZI WATAKIWA KURUDI MAKAMBINI  
NDANI YA SIKU SABA**

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inawatangazia Waomba Hifadhi na Wakimbizi wote waliopewa Hadhi na Hifadhi ya ukimbizi hapa nchini kwa Mujibu wa Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya Mwaka 1998 ambao wapo nje ya kambi za wakimbizi za Nyarugusu, Nduta na Mtendeli zilizopo mkoani Kigoma kurudi mara moja makambini kama Kifungu cha 17 cha Sheria ya Wakimbizi kinavyowataka.

Muomba Hifadhi na Mkimbizi yeyote aliyepo nje ya kambi aliyopangiwa kuishi anapaswa kurudi kambini ndani ya siku saba (7) tangu kutolewa kwa tangazo hili, na kwa yeyote atakaye kaidi agizo hili, atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kupelekwa mahakamani ama kifungo kisichozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au vyote kwa pamoja kama Kifungu cha 24 (2) cha Sheria ya Wakimbizi kinavyotamka.

Taasisi na wananchi wote ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakiwahifadhi nje ya kambi Waomba Hifadhi na Wakimbizi kinyume cha Sheria wanatakiwa kuwarudisha Kambini mara moja ndani ya siku saba (7) kinyume cha hapo sheria itachukua mkondo wake.

Aidha, Tangazo hili halitawahusu Waomba Hifadhi na Wakimbizi ambao wana vibali halali vya kuwa nje ya kambi kwa sababu mbalimbali kama matibabu au masomo.

  
Meja Jenerali J. G. Kingu, ndc  
**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**